**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI**

**YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Mawasiliano**

**Mkuu wa Shule 0752916826**

**Makam Mkuu wa shule 0746620939**

**Matron 0746379425**

**Shule ya Sekondari DR. Samia S.H**

**S.L.P. 73, TUNDUMA.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI DR. SAMIA S.H. HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA MKOA WA SONGWE MWAKA…………………………**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka……………………na atasoma tahasusi ya …….……..........
Shule ya Sekondari DR. Samia S.H ipo umbali wa Kilometa 12 Kaskazini mwa Mji wa Tunduma kutoka kwenye makao makuu ya Mji.

Usafiri kutoka standi kuu ya mabasi ya Mji wa Tunduma Nauli ni Shilingi 500/= kwa basi na 1000/= kwa bajaji, hadi Chapwa Standi. Utapanda Pikipiki hadi shuleni kwa nauli ya Shilingi 5000/= kwa pikipiki.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe itakayotangazwa na Serikali.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare za shule hii ni sketi za vitambaa vya draft zenye mshono wa rinda box mbele na nyuma, pembeni kulia na kushoto marinda manne ya kawaida. Sare hizo zinapatikana shuleni endapo kutakua na changamoto yoyote katika upatikanaji kwa gharama ya shilingi 60,000/= kwa sketi zote mbili pamoja na tai zake

ii. Mashati meupe mawili ya mikono mirefu. (Unaweza kupata shuleni kama hujayapa huko unakotoka kwa gharama ya 15,000/=)

iii. Kwa waislam watavaa hijab ya rangi nyeupe inayofunika kifua cha mwanafunzi, pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama. (Aje nazo mbili)

iv. Trucksuit mbili, moja ya dark bluu na nyingine ya kijivu zenye mistari ya rangi nyeupe pembeni na raba nyeusi jozi moja.

v. Tisheti (T-shirt) mbili, moja ya rangi ya kijivu na nyingine ya rangi ya dark blue. Ukishindwa kuzipata zinaweza kupatikana shuleni kwa gharama ya shilingi 14,000/= kwa kila moja.

vi. Viatu vya shule ni jozi mbili nyeusi vya kufunga na kamba venye visigino vifupi aje navyo

vii. Soksi jozi mbili nyeupe ndefu, sweta la shule jozi mbili nyeusi yenye shingo ya V na mkono mirefu. Aje nazo.

viii. Nguo za kushindia ***shamba dress*** (gauni) rangi ya Dark blue yenye mshono wa solo na iwe ndefu kukaribia kiwiko cha mguu na iwe ya mikono mifupi na kwa waislam mikono mirefu. Aje nayo

### 2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -

i. Madaftari tisa makubwa (Q3 AU Q4)

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology

v. Scientific Calculator kwa wanafunzi wa sayansi na masomo ya geografia

vi. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni lenye ukubwa wa ft 2.5x6

vii. Mashuka Jozi 2 yenye rangi ya pink na bluu bahari, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 nyeupe.

ii. Nguo za ndani za kutosha.

iii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe vyombo hivyo kasoro kijiko viwe vya rangi ya kijani);

iv. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko, mopper yenye kindoo chake kwa ajili ya kudekia na squeezer

v. Sabuni ya maji kwa ajili ya usafi lita tano

vi. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani(soft broom) na hard brooms.

i. Dumu la lita tano kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB: michango yote iingizwe kwenye account namba 0150755126000 CRDB BANK Jina la account DR. SAMIA S.H SECONDARY SCHOOL**

**NB: KILA MWANAFUNZI AKUMBUKE KUJA NA BIMA YA AFYA KWA AJILI YA KURAHISISHA GHARAMA ZA MATIBABU PINDI AWAPO HAPA SHULENI.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**
   i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
   ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
   iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
   iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
   v. Birth certificate na
   vi. Leaving certificate ya kidato cha nne.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule: ANNA SALUTARY MUSHI**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0752916826**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0746 620 939**
- **Mwandamizi Taaluma 0769 028 454**

**MUHIMU SANA**

- **MWANAFUNZI AJE NA BIMA YA AFYA NA KAMA HANA ATATAKIWA KULIPIA MOJA KWA MOJA SHULENI SIKU YA KURIPOTI KIASI CHA SHILINGI ELFU HAMSINI NA MIA NNE TU (TSH. 50,400/=)**
- Kwa bima hii itamwezesha mwanafunzi kupata matibabu ya aina yoyote ikiwepo vipimo na dawa pindi auguapo akiwa shuleni nan je ya shule wakati wa likizo na katika hospiali zote kuanzia ngazi ya wilaya, mkoa, kanda na hospitali zote za rufaa.
- Ikumbukwe pia bima hiyo itadumu ndani ya mwaka mmoja na fedha hiyo italipwa shuleni kwa control number.

**PRIME MINISTER'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

DR. SAMIA S.H. SECONDARY SCHOOL

P.O. Box 73

**TUNDUMA.**

Date: ………………………………

To:

**THE MEDICAL OFFICER,**

……………………………………..

……………………………………..

Please examine ……………………………………………………………….

As to her fitness for pursuing further education at this school.

- Hemoglobin ……………………………………………………………………...
- P.V. Blooding……………………………………......
- (A) Blooding ………………………………………
  (B) Hearing ………………………………………
- Blood Pressure……………………………………
- Urine for Sugar and Pregnancy tests……………………….
- Stool for routine examination…………………………………….
- Asthma ……………………………………………………….
- Skin diseases …………………………………………………
- Leprosy ……….………………………………………
- Pulmonary tuberculosis ……………………………………….
- Employs …………………………………………………….
- Deformity ……………………………………………
- Mental problem……………………………………………
- Comments ………………………………………………………………

……………………………………………

**DESIGNATION**

**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**
**SHULE YA SEKONDARI DR. SAMIA S.H.**
**FOMU YA KUKUBALI NAFASI**

**a. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI (ijazwe na mwafunzi mwenyewe)**

Jina kamili [kama alivyo sajiliwa darasa la saba]…………………………………………………
Tarehe ya kuzaliwa…………….…Kabila…………………dini na dhehebu……………………

shule nitokayo…………….…………Mahali niishipo…………………………..

Mkoa……………………….…Anuani…………………………………………

Jina la baba/mlezi……………………………………….kazi yake…………………………..

Jina la mama/mlezi……………………………………...kazi yake……………………………

Wazazi/walezi wanaishi (wapi)…………………………pamoja/au wametengana……………

Anuani ya mzazi/mlezi……………………………..simu……………………………………

Wakati wa likizo nitakuwa kwa (mtaje)……………………………wapi………………………

Nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli na sahihi;

Sahihi ya mwanafunzi………………………………tarehe……………………………….

KUKUBALI (mwanafunzi mwenyewe ajaze)

Mimi……………………………………………………………………………nimesoma maagizo kwa makini na kuzielewa taratibu za shule na nipo tayari kuzifuata. Hivyo ninakubali nafasi niliyopewa na nitafika shuleni tarehe iliyopangwa.

**b. IJAZWE NA MZAZI AU MLEZI**

Mimi………………………………………………………………. ambaye ni ……………………………. wa mwanafunzi huyu nimesoma kwa makini maelekezo pamoja na sheria za shule katika fomu ya kujiunga. Nipo tayari ajiunge na shule hii, naahidi kumpa mahitaji yote ili aweze kupata elimu yake vizuri katika shule hii. Aidha nitasaidiana na walezi wa shuleni katika kumlea mwanafunzi huyu katika maadili mema na kuitikia wito wa kufika shuleni pale nitakapohitajika.

Anuani yangu ya kudumu……………………………..simu………………………………

Nikipata uhamisho ama kubadilisha makazi nitaijulisha shule kwa maandishi.

Nathibitisha Taarifa nilizotoa ni sahihi na kweli

Sahihi ya mzazi /mlezi………………